

Shirika la Kimataifa la Msalaba Mwekundu na Hilali Nyekundi (IFRC)

Mwongozo ya Kipindi ya Redio ya Virusi ya mupya ya Corona na mipango ya Matangazo

Mawasiliano ya hatari na ahadi ya jamii juu ya virusi ya mupya ya corona

Nakala: 15/03/2020

Sababu

Redio inafanya kazi ya lazima mukufikisha taarifa za habari kwa jamii yenye iko mbali sana na kubapatia habari za kubasaidia kujikinga mu maisha wakati za hali za hatari. Pia ni jukwaa ya ku himiza maoni wazi na maoni kuhusu maneno za mingi za lazima. Redio inaesababishwa mara kwa mara na jamii mu dunia muzima na mu Afrika kama njia moja ya kuaminika zaidi na yenye inatumikishiwa sana kwa mawasiliano na kuifanya kuwa njia nzuri ya jamii kuwasiliana juu ya virusi ya mupya ya corona. Sababu ya iyi mawasiliano ya hatari na ushiriki ya jamii (RCCE) ni kukusaidia kufanya kipindi ya mashirikiano katika redio juu ya kupatia jamii taarifa za habari za sasa, za ukweli kuhusu virusi ya mupya ya corona. Sababu ya iyi mawasiliano ya hatari na ushiriki ya jamii (RCCE) ni kukusaidia kufanya kipindi ya mashirikiano katika redio juu ya kupatia jamii taarifa za habari za sasa, za ukweli kuhusu virusi ya mupya ya corona. Inaweza pia kutumikishiwa kukusanya maoni kutoka kwa jamii juu ya ufahamu, maulizo, maombi na habari za bongo zenye zinazunguruka katika jamii kuhusu virusi ya mupya ya corona na kugombanisha taarifa za habari za bongo.

Ni nini kipindi ya mashirikiano ya redio?

Kipindi ya mashirikiano ya redio ni mazungumzo ku redio, kawaida ya kufanya karibu saa moja, yenye iko amo mazungumzo na mugeni (bageeni) mwenye anajuwa zaidi kuhusu ile mambo na wakati kwa wasikilizaji kupiga simu au kutuma message zenye ziko amo maulizo na maoni zenye zitajibiwa na ule mugeni (bageeni) mwenye anajuwa zaidi. Maulizo zenye zinaulizwa kwa bageni wakati ya kipindi ya mashirikiano zinakuwaka wazi, kwa ju ya kupana taarifa ya habari yenye iko wazi, zenye zinaweza shikiwa na kusukuma wasikilizaji kupiga simu na kupana ufahamu yabo, imani, wasiwasi, maulizo na maoni. Kipindi kinaweza kuwa amo pia mazungumzo yenye balirikodi mbele paamoya na batu ya mu jamii (vox pops), muziki, michezo, bu ma publicités kuhusu virusi ya mupya ya corona.

Unahitaji nini kwa kufanya kipindi ya mashirikiano ya redio?

Kwa kufanya kipindi ya redio ya mashirikiano unahitaji station ya redio yenye itakuwa napita ako, batu na vyombo.

Station ya redio

Njia ya rahisi na ya haraka sana ya kutangaza kipindi ya redio ya mashirikiano ni kutumika na station ya redio yenye ilishaka kuwa na kuuza wakati ya kupitisha kipindi yako. Kama hauya hauyashirikiana na station ya redio ata moya, unapashwa chagula station yenye inasikilizwaka sana na basikilizaji benye uko natafuta, yenye inaaminika na batu, yenye inatangazaka mu luga yenye basikilizaji bako banapendaka na yenye haina ushirika mkubwa na kikundi ata kimoja, kwa mfano za kidini au za kisiasa. Inawezekanaka mara mingi kusikilizana beyi ya muzuri kwa muda wa redio kwa kuonesha kusudi ya kibinadamu ya ile kipindi ya redio.

Batu

Kunakuwaka aine ine ya batu benye banahusika katika kipindi ya mashirikiano ya redio; mutangazaji, mugeni (bageeni), Batayarishaji na basikilizaji.

Mutangazaji anapashwa:

- ✓ kuwa na mazoezi ya batangazaji ba redio
- ✓ kuzungumza luga ya mu ile fasi
- ✓ kujuwa kuongea, kuweza kufurahisha bageeni na basikilizaji
- ✓ kujuwa kufanya maulizo muzuri
- ✓ kutopendelea na kuheshimu maoni ya batu
- ✓ kuweza kufanya kazi za mingi kwa limoya, kuongea na bageeni, kupokea simu kutoka kwa wasikilizaji na kuchunga muda isipitishwe
- ✓ kujuwa habari za sasa na za ukweli kuhusu virusi ya mupya ya corona.

Mugeni (bageeni) anapashwa:

- ✓ kuwa mufanyakazi wa afya, mwenye anajuwa sana kuhusu virusi ya mupya ya corona, kuchanga na ma alama, maambukizi, gisi ya kutunza na bingine. Mugeni (bageeni) anapashwa kuweza kugombanisha habari za bongo mu kusema ukweli
- ✓ kutokea ku shirika yenye inaaminika ao kikundi yenye inatimilika sana mu bya afya. Kwa mfano, mutu wa Msalaba Mwekundu (croix rouge) na Hilali Nyekundu, shirika ya afya duniani (OMS) ao ministere ya Afya
- ✓ kuwa na busikilizaji ya muzuri na kuonesha huruma kwa basikilizaji
- ✓ kuwa na uwezo wa kusema wazi na kueleza habari za kiufundi za afya mu maneno zenye zina sikilikana.

Batayarishaji banapashwa:

- ✓ kufahamu gisi ya kuongoza kipindi ya redio na viombo, kwa mfano mitambo
- ✓ uwezo wa kubadirisha kati ya bitu tafauti; muziki, publicités, vox pops, mutangazaji na wakati ya kupiga simu
- ✓ kuongoza muda
- ✓ kuongea wazi na mutangazaji

Mara mingi ya muzuri ni kulomba msaada ya mtayarishaji wa redio mwenye anabijuwa sana mwenye anatumikaka ndani ya station ya redio yenye unatangiaka ako.

Viombo

- ✓ kufuatana na station ya redio yenye unafanya kazi nayo, unaweza kuhitaji simu ya mkononi ya kupokea simu kutoka kwa wasikilizaji. Ya muzuri inapashwa kuwa bure kwa wasikilizaji kupiga simu ao kutuma message zabo mu kipindi
- ✓ ukipanga kufanya maongezi yenye bali rekodi na wasikilizaji utahitaji dictaphone na ordinateur kwa kubi badirisha.

Maongozo za kufanya kipindi ya redio

| Matayarisho | Mbele ya kipindi | Wakati ya kipindi |
|--|---|---|
| <ul style="list-style-type: none"> ✓ Tafuta ma habari kuhusu bienye utaongea ako na utayarrishe ujumbe (message) ya lazima yenye unataka kushiriki na wasikilizaji ✓ Tafuta mugeni mwenye anakamilika ✓ Tayarisha maulizo zako ✓ Kutana na mugeni wako na muongeye ju ya maulizo mbele na ujumbe ya lazima ya wasikilizaji ✓ Tayarisha maulizo kwa vox pops, kama munaifanyaka. Kwa mfano, Umesikia nini kuhusu virusi ya mupya ya corona?' ao batu banaweza kupata virusi ya mupya ya corona aye?' ✓ Fanya ma vox pops zako na kisha uzitengeneze muzuri ju zikuwe tayari kwa kipindi ✓ Panga gisi ya kupokea simu na ujumbe (message) kutoka kwa wasikilizaji na ununuwe simu ya mkononi ikihitajika. | <ul style="list-style-type: none"> ✓ Fanya mipango za kuinuwa kipindi ya redio kwa wafanyakazi, wanaojitolea na jamii kupitia njia yoyote yenyi unaweza kuwasiliana amo na izi vikundi. ✓ Jipatie muda ya mingi ya kufikio ku studio bila haraka ✓ Hakikisha umepata kila kitu kienye unahitaji; mipangilio ya kipindi na maulizo, vox pops zilizorekodiwa na ma publicités ✓ Zungumza kuhusu mipangilio ya kipindi na mtayarishaji wa vipindi ✓ Chunguza kama biombo biako byote binatumika na kama unajua gisi ya kutumikisha micro. | <ul style="list-style-type: none"> ✓ Tiya ecouteur ku lisikio moja uendelee kuzungumza na b bila magumu ✓ Kuwa na kalamu (bic) na ka tayari ✓ Ujitambulish na utambulish kipindi kila mara ✓ Utambulish bageni bako ✓ Eleza nia na bienye bitafany wakati ya kipindi ✓ Omba mugeni wako ajibu ul tena kama jibu yake ya kwa haiko wazi ao umukate kifup kama anazungumza muda murefu sana. Kazi yako ya kwanza ni kwa wasikilizaji ✓ Hakikisha uliachiya muda ya kutosha kwa basikilizaji bak kupiga simu ✓ Mara kwa mara bape nume simu yenye basikilizaji bana kutumikisha kupiga simu, ku ujumbe (message) ao Whats na maulizo zabo na maoni ✓ Andika maulizo zote, maom maoni zenye zilitolewa na basikilizaji benye balipiga si katika kipindi. |

Mipango za vipindi ya Redio: Virusi ya mupya ya corona

Kumbuka: mupango iyi ya kipindi ya redio iko na nia ya kufanya kazi ju batu bote baelewe virusi ya mupya ya corona ni nini. Bipindi bya siku zingine zinaweza kuzingatia zaidi ubaguzi, kujitenga mwenyewe, ma habari za bongo zimoya na bingine.

Tarehe:

Swali:

Jina ya watangazaji:

1.

2.

Jina za mugeni (bageeni):

1.

2.

| Wakati | Muda | Bienye biko mu ndani |
|--------|-------|--|
| 00:00 | 45" | Publicité ya kuanza |
| 00:45" | 2' | <p>Mwanzo ya kipindi:</p> <p>Tambulisha swali: Tuko hapa leo kuzungumza juu ya virusi ya mupya ya corona. Pa vyombo vya habari, mtandao (internet), jamii na bikundi, batu ba mingi bamechangan leo tunaenda kutoa ukweli kuhusu:</p> <ul style="list-style-type: none"> • Virusi ya mupya ya corona ni nini na ni hatari kiasi gani? • Gigi virusi inasambaranaka? • Tunaweza fanya nini kwa kujikinga? • Ni bongo gani yenyi iko nazunguka kuhusu virusi ya corona - na ukweli ni ya <p>Kujibu izi maulizo itatusaidia kuelewa corona na kuhakikisha tunajua nini tunawez kufukuza boga zimoya na wasiwasi juu ya virusi.</p> |
| 02:45 | 2' | Tambulisha bageeni: Majina, kazi zabo na bikundi biabo |
| 04: 45 | 0.30" | Muziki |
| 05:15 | 1'30 | Cheza vox pops pamoja na maoni na maulizo kutoka kwa wanajamii |
| 06:45 | 2' | Bageeni banajibu Vox pops |
| 08:45 | 10 | <p>Maulizo kwa bageeni</p> <p>Q1: Virusi ya mupya ya corona ni nini?</p> <p>Q2: Iyi ugonjwa ni hatari namna gani? Batu ba mingi banakufaka nayo?</p> <p>Q3: Inalingana aye na homa ya kawaida ao mafua?</p> <p>Q.4: Ma alama za virusi ya corona ni gani?</p> |
| 18:45 | 0.30" | Muziki |
| 19:15 | 45" | Cheza vox pops pamoja na maoni na maulizo kutoka kwa wanajamii |
| 20:00 | 2 | Bageeni banajibu Vox Pop |
| 22.00 | 12' | <p>Rudi kwenye maulizo zaidi</p> <p>Q5: Virusi ya mupya ya corona inaambukiaka aye? Inaweza kuambukizwa kupitia he</p> |

| | | |
|---------|------|---|
| | | <p>Q.6: Tunaweza kufanya nini kwa kujikinga na virusi ya corona?</p> <p>Q.7: Minapashwa kuvala maski kwa kujikinga mwenyewe?</p> <p>Q.8: Minapashwa fanya nini kama mimi ao ndugu yangu iko na ma alama?</p> <p>Q.9: Kuko batu benyi biko mu hatari zaidi kwa virusi ya corona kushinda bengine?</p> |
| 34.00 | 1' | Omba wasikilizaji wapige simu, watume ujumbe (message) ao WhatsApp na maoni kwa kupiga simu |
| 35.00 | 21' | Basikilizaji banapiga simu: kila mara bakumbushe numero ya kuita |
| | | <p>Maulizo ya kuuliza wakati ukonasubiri bageni bapige simu</p> <p>Q.10: Naweza pata ugonjwa ya virusi ya corona kwa kuzungumza ao kuikala karibu yangu?</p> <p>Q.11: Kuko chanjo, dawa ao matunzo ya virusi ya mupya ya corona?</p> <p>Q.12 Antibiotiki inafaa kuzuia ao tunza virusi ya mupya ya corona?</p> <p>Q.13: Nisalama kupokea muzigo ya kutokea China ao mafasi zingine kwenye virusi ya corona?</p> <p>Q.14: Nini inafikaka kama mutu banamuwazia kukuwa na alama za virusi ya corona?</p> |
| 56.00 | 30'' | Muziki |
| 56.30 | 2' | Kifupi: jumbe za lazima |
| 58.30'' | 1' | Maliza kipindi na upane maelezo ya njia zozote za maoni ya Jumuiya ya Kitaifa za Maoni na kuuliza maulizo. |
| 59.30'' | 30'' | Publicité ya kufunga |
| 60.00 | | Mwisho |

Maulizo na majibu juu ya virusi ya mupya ya corona

Virusi ya mupya ya corona ni nini?

Virusi ya corona ni familia kubwa ya virusi inayopatikana mu ma nyama na binadamu pia. Zimoya zinaambukizaka batu na zinajulikana kusababisha magonjwa kuanzia mafua mbaka magonjwa makubwa kama vile MERS na SARS. Virusi ya mupya ya corona na magonjwa yake (COVID-19) ni ugonjwa ya mupya ya virusi ya corona iliyopatikana kwanza huko Wuhan, mu China mu Disemba (mwezi ya kumi na mbili) 2019. Kungali mambo ingine yenyi hatujuwe kuhusu virusi, lakini batafutaji banafanya kazi kutafuta gisi ya kuizuia na kuiponesha.

Ile ugonjwa kio hatari kiasi gani?

Kama vile na magonjwa zingine za kupumua, kuambukizwa na virusi ya mupya ya corona inaweza sababisha ma alama za kidogo na pia ndani mafua, kigohazi, na homa. Inaweza kuwa makali zaidi kwa batu bamoya na inaweza kusababisha magonjwa ya mafafa (pneumonia) ao shida za kupumua. Haiko ya kawaida iyi ugonjwa iuwe mutu. Bazee, na batu benye hali ya

matatizo ya kiafya (kama vile ugonjwa wa kisukari na ugonjwa ya moyo) banaonekana kukuwa katika hatari kubwa ya kuwa bagonjwa sana kutokana na virusi.

Kuko batu bamingi benye biko nakufa na iyi virusi?

Virusi ya mupya ya corona inasababishaka alama za kidogo ku kiasi ya 80% ya batu banaogunduliwa, na kiasi ya 10% ya batu banaugua ugonjwa makali na 10% banauguwa na ugonjwa ya makali sana benye banahitaji matunzo makubwa. Kati ya 2-3% ya batu ambao banapatikana na ugonjwa banakufaka; hatari ya kifo ni kubwa zaidi kwa bazee, na kwa batu ambao bana magonjwa mengine kama ugonjwa ya moyo, ugonjwa wa moyo (tension) ao ugonjwa wa sukari.

Sababu ya iyi mawasiliano ya hatari na ushiriki ya jamii (RCCE) ni kukusaidia kufanya kipindi ya mashirikiano katika redio juu ya kupatia jamii taarifa za habari za sasa, za ukweli kuhusu virusi ya mupya ya corona. Vipimo ya batu benye biko na virusi ya mupya ya corona benye banakufaka na ile ugonjwa mbaka leo imekuwa tafauti sana kufuatana na hali. Kwa mfano, uwingi ya bifo mbaka leo uko Wuhan ni 2-3%, wakati ni chini ya 1% katika sehemu zingine za Uchina. Bado haiya julikana tofauti inaletwa na nini. Ma kesi za mingi mbaka leo zimetokea katika ma inchi zilizo na uwezo mkubwa wa viombo vya afya, kwa mfano uwezo wa kutoa msaada wa kupumua kwa ma kesi za makali na ngumu. Inawezekana kwamba uwingi ya batu benyi biko na virusi ya mupya ya corona benye banakufaka na ile ugonjwa inaweza kuwa ya yulu katika hali kwenye msaada ya kidogo inapatikana, ao kwenye batu ba mingi biko na shida za msingi za afya kama ugonjwa za kukawiya mu mwili miaka mingi, maambukizo ya ugonjwa, ao malisho mabaya.

Inalingana aye na homa ya kawaida ao mafua?

Hatuwezi kulinganisha uwingi za bifo kwa sababu batu ba mingi benye biko na alama zidogo za mafua habapendake kuenda kwa munganga. Kwa hivyo hatujuwe ni ma kesi ngapi za mafua ao homa zenye zinakuwaka kila mwaka. Lakini mafua inaendelea kuuwa batu inchini Ungereza, gisi inafanyaka kila miezi za baridi (hiver). Amerika imeripoti bifo 10,000 kutoka kwa mafua ya saison wakati ya saison ya mafua ya 2019/2020 na Wamarekani zaidi ya milioni 2 waliguswa. Mashauri kutoka kwa shirika la afya duniani (OMS) ni kwamba unaweza kujikinga na virusi yote ya kupumua uki nawa mikono yako, epuka batu benye bana gohola na kupiga chafya na jaribu kutogusa macho yako, pua na mdomo.

Alama za virusi ya mupya ya corona ni gani?

Alama ya kwanza na ya kawaida ya virusi ya mupya ya corona ni homa. Batu ba mingi pia banapata kigohozi kia kuwasha ku shingo. Izi zinaweza kufuatiwa nyuma na muchoko, maumivu ya mishipa. Kawaida, batu balioambukizwa na virusi banaweza kutoa makamasi ao kugohola damu, ao kupata shida ya kupumua, maumivu ya kichwa, kuchanganyikiwa, ao kuhara. Batu benye banagonjwa na virusi ya mupya ya corona kawaida banapata alama za ugonjwa kati ya siku moja mbaka ku siku 15. Bagonjwa benye bamepata ugonjwa kali ao benye bamekufa banaonekanaka kuanza na ka ugonjwa kadogo na kukuwa bagonjwa sana tena katika juma ya pili ya ugonjwa. Batu benyi biko na ugonjwa kali banaweza hitaji kulazwa hospitalini kwa juma za mingi.

Virusi ya corona inaambukizwaka aye?

Virusi ya mupya ya corona inaweza kuambukia kutokea ku mutu umoja ku mwengine. Virusi zingine za corona zenye zinaweza kuambukia kutokea ku mutu umoja mbaka ku mutu mwengine

kwa kawaida inaambukiaka kwa njia ya kugusana na batu benyi biko na ma alama za ugonjwa, ao kupitia kugusa ma toni za mate yabo, maji ingine ya mwili ao mavi, yenyi inaweza kuwa na virusi. Ushuhuda ya sasa ya muripuko ya virusi ya mupya ya corona inaonesha kama ma toni na kugusana na mutu aliyeambukizwa ao kitu kienye bamegusa inaweza kuwa sababu ya uwingi ya maambukizi.

Kugusa ma toni yenyi inatoka wakati mutu mwenye iko na virusi ya mupya ya corona anagohola ao kupiga chafya, gisi ma toni ya mate ao ingine maji ya mwili zinazobeba virusi zinazoelekezwa kwa batu bengine ao bitu byenye mutu mwengine atagusa baadaye;

- Kugusana ya karibu, kama kugusana, kusalimiana na mikono, ao mgusano wa kingono
- Kugusa kitu ao sehemu ambapo virusi imewekwa, kama vile kwa kufungulia mulango ao mali ya kibinafsi, kisha kugusa mdomo wako, pua, ao macho bila kwanza kunawa mikono yako
- Virusi zingine ya corona, kama SARS-CoV, zinaweza kupatikana mu mavi za batu balioambukizwa na virusi na zinaweza kusambarana kwa kugusana na majimaji hayo. Haiya fahamika wazi kama virusi ya mupya ya corona inaweza kuambukizwa kupitia njia ya mavi - mdomo, lakini mbaka siku tutajuwa bengine ni muzuri kuishi sawa gisi inawezekana.

Kuko ushuhuda fulani kwamba batu banaweza kuambukiza virusi ata kama onekana ako ma alama za ugonjwa; ile ushuhuda ya sasa inaonesha kama kugusana na batu benyi biko na alama za ugonjwa njo njia ya kwanza ya muripuko. Visa vingi vinavyojulikana vinahusu mgusano wa moja kwa moja na mtu ambaye tayari anaonesha dalili za virusi mpya ya corona, kama vile joto jingi ao kukohoa.

Je, kipindi ya kupevika ni muda gani?

Ushuhuda wa sasa unaonesha kama kipindi ya kutoka kusiku mutu aliambukizwa mbaka ku siku yenye alama zinaanza onekana ni siku 5-6 (kuanzia siku 2-14). Hesabu ya sasa inaonesha kama kila mtu anayepatikana na virusi mpya ya corona anaweza kuambukiza kwa zaidi ya watu wawili, ambayo inamaanisha kwamba muripuko ineza endeleva kukua kwa kukosekana kwa hatua za kujikinga.

Je, tunaweza kufanya nini kujikinga dhidi ya virusi vya corona?

Mambo matano ya kufanya;

- Osha mikono yako kila mara kutumia sabuni na maji. Ikiwa sabuni haipatikani, jivu au jeli ya mikono iliyotengenezwa na pombe inaweza kutumika kuosha vijidudu.
- Ukikohoa ao kupiga chafya, funika mdomo wako au pua na kiwiko chako ao tishu. Jaribu kutokohoa na kupiga chafya mikononi mwako kwa sababu utaeneza virusi kwa mikono yako. Tupa tishu kwa pipa la taka. Ikiwa unakohoa / kupiga chafya mikononi mwako, usiguse kitu chochote na safisha mikono yako mara moja kwa sabuni na maji.
- Epuka kuwasiliana na mtu yeyote anayekohoa, kupiga chafya, au mgonjwa. Weka umbali wa angalau mita 1 (miguu 3) na uwahimize waende katika kituo cha huduma za afya kilicho karibu.

- Epuka kugusa macho, pua na mdomo. Mikono inagusa vitu vingi vinavyoweza kuambukizwa na virusi.
- Tembelea daktari ukiwa na homa ya mingi, kikohozi ao unasikia matatizo ya kupumua. Hii ndio njia bora ya kujitunza na kuzuia maambukizi kuenea kwa familia yako na wengine. Hakikisha umempigia simu daktari kwanza na umjulisha alama zako za ugonjwa ili usiwaambukize batu bengine.

Je, itaomba kuvala mask ili kujikinga?

Watu wasio na alama za magumu ya kupumua, kama kikohozi, hawahitaji kuvala mask. OMS inashauria utumiaji wa mask kwa batu ambao biko na alama za virusi mpya ya corona na kwa bale banaotunza batu balio na dalili, kama kikohozi na homa. Matumizi ya mask ni muhimu kwa wafanyakazi wa afya na batu ambao banaangaikia mtu (nyumbani au katika kituo cha utunzaji wa afya).

Tumia mask ikiwa tu uko na alama za magumu ya kupumua (kukohoa ao kupiga chafya), kama unawaza kama umeambukizwa na corona na alama za kidogo, ao unamtunza mtu mwenye unawaza iko na maambukizi ya corona. Virus mpya ya corona inaambatana na kusafiri katika maeneo ambayo ma kesi zimesemeka kama ziko, ao magusano ya karibu na mtu ambaye amesafiri katika maeneo haya na amegeuka mgonjwa.

Njia za muzuri zaidi za kujikinga na bengine na corona ni kunawa mikono yako mara kwa mara, funika kikohozi yako na mukunjo ya ndani ya konongo yako ao kitambala na ubakie mabli ya metre moja (fiti 3) na watu wanaokohoa ao kupiga chafya.

Je, nifanye nini kama ndugu yangu ao mimi niko na ma alama za ugonjwa?

Tafuta mbiombio matunzo kama wewe ao ndugu yako iko na homa, kikohozi ao matatizo ya kupumua.

Ita ku simu munganga wako ao mhudumu wa afya mbele ya kuenda ku kliniki. Unapashwa pia kupiga simu kama umesafiri katika eneo ambayo ugonjwa ya virusi mpya ya corona (corona) imesemewa iko, ao kama umegusana kwa karibu na mtu ambaye amesafiri kutoka mu moja ya izi maeneo na iko na ma alama za ugonjwa

Batu bamoya biko mu hatari kubwa ya corona kushinda bengine?

Wakati bado tunajifunza juu ya gisi virusi mpya ya corona iko na sumbuwa batu, bazee na batu benye hali ya mubaya ya afya (kama vile ugonjwa ya moyo, ao ugonjwa wa sukari) banaonekanaka kugonjwa sana kushinda bengine.

Naweza kupata ugonjwa ya virusi mpya ya corona (virusi mpya ya corona) kwa kuzungumza na mtu ao kuikala karibu naye?

Hakuna uwezekano kupata virusi kwa kuongea na batu, kutembea barabarani, ao kuenda sokoni ao kwenye batu ba mingi biko. Kukuwa karibu ya mtu kawaida haiwezi kuambukizia virusi. Hakuna uwezo ya kupata virusi kama hauku safiri kuenda mu inchi zenye ugonjwa iko amo kwa sasa ao kama haugusane na mtu ambaye ni mgonjwa wa corona

Ni salama kupokea muzigo ya kutokea China ao mafasi zingine?

Ndiyo. Uwezo wa mtu kuambukiza muzigo za biashara ni ya kidogo na hatari ya kupata virusi ambayo inasababisha virusi mpya ya corona kutoka kwa muzigo ambayo imeletwa, kusafiri, na kutolewa kwa hali tafauti ya joto pia ni ya chini.



Kuko chanjo ao dawa ya tunza virusi mpya ya corona?

Hakuna chanjo ao dawa ya kuzuia ao kutunza virusi mpya ya corona. Utunzaji wa kusaidia unapendekezwa kwa batu benye baliambukizwa kuondoa ma alama. Upimaji katika laboratoire inaweza hakikisha kama mtu iko na virusi mpya ya corona.

Antibiotiki inafaa kuzuia ao kutunza virusi mpya ya corona?

Apana. Antibiotiki haizuiye virusi, zinafanya kazi tu ku maambukizi ya (vidudu ya mu mwili) bakteria. Virusi mpya ya corona inasababishwa na virusi, kwa hiyo antibiotiki haitumike. Antibiotiki haipashwe kutumikishwa sawa vile njia ya kuzuia ao kutunza ugonjwa ya virusi mpya ya corona. Zinapashwa kutumikishwa tu kama ilivyoshauriwa na daktari kutunza maambukizi ya bakteria.

Nini inapitikana wakati mtu anafanana kukuwa na alama za virusi ya corona?

Ushuhuda wa sasa unaonesha kama kipindi ya kutoka kusiku mutu aliambukizwa mbaka ku siku yenye alama zinaanza onekana ni siku 5-6 (kuanzia siku 2-14). Hesabu ya sasa inaonesha kama kila mtu anayepatikana na virusi mpya ya corona anaweza kuambukiza kwa zaidi ya watu wawili, ambayo inamaanisha kwamba muripuko ineza endeleya kukua kwa kukosekana kwa hatua za kujikinga. Kila mtu mwenye banawazia kukuwa na virusi ya corona anapashwa kutafuta mashauri ya kiafya na kujitenga mwenyewe.